**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAOMBI YA BAJETI YA ZIADA (SUPPLEMENTARY BUDGET) KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA AJILI YA UJENZI WA MASOKO YA MWANAKWEREKWE, JUMBI NA CHUINI

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuendelea kutukarimu neema zake zisizo na kifani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yetu mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kukushukuru wewe binafsi, pamoja na wasaidizi wako Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa uongozi wenu mahiri katika kipindi chote ambacho tunakutana kwa ajili ya kujadili mambo mbali mbali. Aidha, shukurani zangu za dhati ziende kwa Wajumbe wa Kamati ambao walinisaidia kwa karibu kufanikisha majukumu yetu na kuweza kuwasilisha maoni yetu mbele ya Baraza lako.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe wa Kamati na Makatibu kama ifuatavyo;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 8. | Ndg. Abass Vuai Mohammed | Katibu |

9. Ndg. Husna Rajab Othman — Katibu na
10. Ndg. Shaib Fadhil Shaib — Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo, napenda kuliarifu Baraza lako kwamba, Kamati ya Bajeti ilikutana na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango pamoja na Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa lengo la kujadili Maombi ya Bajeti ya Ziada (Supplementary Budget) itakayotumika kujenga masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.

**Mheshimiwa Spika,** Ifahamike kuwa, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Baraza la Wawakilishi liliidhinisha TZS 17.60 bilioni kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kuwa, awali Serikali ilitarajia kufanya ujenzi wa masoko kwa njia ya mashirikiano na Sekta Binafsi, lakini kutokana na sababu mbali mbali zilizojitokeza zilizopelekea kutokujengwa kwa masoko hayo, Serikali iliamua kuendelea na mradi wa ujenzi wa masoko kupitia mkopo kutoka CRDB wa TZS 16.28 bilioni.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa kuletwa Maombi haya ya Bajeti ya Ziada ni kutokana na kuongezeka kwa matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini ambapo matumizi hayo awali yalipangwa kutekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Nyongeza hii itapelekea kubadilika kwa Sura ya Bajeti kutoka TZS 2,590.30 na kufikia TZS 2,606.58.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilikubaliana na nyongeza ya TZS 16.28 bilioni kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Kamati kukubaliana na Maombi haya ya Bajeti ya Ziada, Kamati inaishauri Serikali kuonesha muda halisi wa mkopo pamoja na riba yake hadi mkopo utakapomaliza kulipwa ili kuweza kufahamu kwa kina gharama zote.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vile Miradi ya Ujenzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini imechelewa kutekelezwa, Kamati inaishauri Serikali kusimamia miradi hiyo na kuhakikisha inakamilika katika muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa

na Idara Maalum za SMZ kuvisimamia kwa karibu Vikosi vya SMZ vilivyokabidhiwa kazi za kutekeleza Miradi hiyo ya Ujenzi wa Masoko pamoja Mshauri Elekezi ambae ni Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa utaratibu uliyo sahihi ikiwemo kufanya vikao vya ujenzi (site meetings) kwa muda.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Maombi ya Bajeti ya Ziada ya Serikali za Mitaa. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza pamoja na Wajumbe wote wa Baraza kwa ushiriakiano wao walioipatia Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Sasa niwaombe Wajumbe wako wayajadili kwa kina Maombi ya Bajeti ya Ziada ya Serikali za Mitaa kwa kutoa mawazo yao katika kuimarisha utekelezaji wa bajeti na hatimae kuipitisha Bajeti ya Ziada (Supplimentary Budget) kwa lengo la kuiwezesha Serikali kufanya matumizi na kukamilisha ujenzi wa masoko na kuwawezesha wananchi kufanya biashara zao katika mazingira bora na kujiongezea kipato chao na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

Mhe. Abdulla Hussein Kombo,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**